JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Shule ya sekondari ya Dutwa
S.L.P 288
Bariadi
14/5/2018

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi .....
S.L.P.....
.....

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DUTWA HALMASHAURI YA WILAYA YA BARIADI MKOA WA SIMIYU MWAKA 2018.**

Nafurahi kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano(V) katika shule hii mwaka 2018 Tahasusi ya **PCM/HKL**

Mahali shule ilipo

Shule ya sekondari Dutwa ipo mkoa wa Simiyu wilaya ya Bariadi vijijini kilomita 30 kutoka kituo cha mabasi Bariadi kuelekea barabara kuu ya Mwanza/Lamadi hadi Dutwa.

Ufikapo Dutwa shule iko Kusini Magharibi mwa senta ya Dutwa,umbali wa nusu kilomita kutoka senta ya Dutwa unaweza kutembea kwa miguu au Pikipiki kufikia shule ilipo

Mhula wa masomo unaanza **tarehe 2/7/2018** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti tarehe **1/7/2018**. Mwisho wa kuripoti ni **tarehe 16/7/2018**

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

SARE YA SHULE

1. Shati mbili aina ya tetroni mikono mifupi zisizobana na ziwe ndefu(kama ni muislamu ashone shati liwe lenye mikono mirefu na Hijabu rangi nyeupe)
2. Viatu vya shule vya ngozi jozi mbili (2) ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
3. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili(2)
4. Sweta la rangi ya Bluu au unaweza kulipata shuleni kwa shilingi 12,000/= . usije na koti wala jaketi

Scanned by CamScanner

5. Tisheti shughuli za nje itakuwa na kola rangi ya Bluu au unaweza kuipata shule kwa Tsh 10,000/=
6. Sketi mbili za darasani rangi ya Bluu bahari ndefu inagusa kisigino au utazipata shuleni kwa Tsh 28,000/=@14,000/=
7. Gauni mbili za kushindia baada ya kutoka darasani rangi ya pinki au utazipata shuleni Tsh 26,000/= @ 13,000/=
8. Nguo za ndani za kutosha

ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) Ada ya shule kwa mwaka ni **Tsh 70,000/=** unaweza kulipa kiasi cha Tsh **35,000/=** kwa muhula.Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule jina la akaunti Dutwa secondary school revenue collection **Na. 3051100018** benki ya **NMB**(tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)

b) **Michango mingine**

i. Tsh 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Tsh 6000 kwa ajili ya kitambulisho na picha
iii. Tsh 20,000/= kwa ajili ya taaluma
iv. Tsh 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi na walinzi
v. Tsh 2000/= Nembo ya shule
vi. Tsh 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza
vii. Tsh 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima
viii. Fedha ya Tahadhali 5000/= (haitarejeshwa)

c) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta**

1. Ream ya karatasi moja kwa mwaka
2. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
3. Scientific calculator kwa wanafunzi wa **PCM**
4. Mashuka pair mbili(2) rangi ya Bluu bahari,Blanket 1,Foronya 1,Chandarua 1.
5. Godoro dogo futi 2½ jipya
6. Taulo 1
7. Pair ya Kitenge 1 au Khanga
8. Dawa ya meno ,Mswaki na sabuni za kutosha
9. Madaftari makubwa ya kutosha (4 quires)
10. Vyombo vya vyakula sahani,bakuri ,kikombe na kijiko (vyombo viwe vya udongo na sio plastic wala shaba)
11. Ndoo 1 kubwa na beseni 1 la kufulia na kuogea
12. Kwanja 1,jembe 1 lenye mpini ,reki 1 yenye mpini ,mifagio ya ndani 1na nje 1

Scanned by CamScanner

Vifaa vya michezo

i. Track suit ya rangi nyeusi yenye michirizi myeupe 1
ii. Tisheti ya njano 1
iii. Raba rangi nyeupe

Njoo na fedha kwa matumizi yako binafsi kwa muhula mzima.

Wajibu wa mwanafunzi

i. Kuamka asubuhi na mapema na kila unapohitajika
ii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
iii. Kuvaa sare ya shule wakati wote kuhudhuria masomo siku zote za masomo
iv. Kuepukana na utoro na uzembe,udanganyifuna uhuni wa kila aina
v. Kuwa na nidhamu ya hali ya juu mahali popote
vi. Kushiriki kikamilifu katika kazi za shule michezo na utamaduni
vii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo shuleni wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
viii. Kushiriki katika shughuli zote zinazokujenga kuwa raia mwema
ix. Mwanafunzi sharti aonekane nadhifu wakati wote
x. Mwanafunzi haruhusiwi kupaka kucha rangi,kupakaa rangi mdomoni na kutunza kucha ndefu wakati wote ukiwa shuleni unatakiwa kuzingatia wajibu wako kama mwanafunzi.Unatakiwa kudumisha amani,nidhamu,ushirikiano,utendaji kazi kwa heshima na kwa kila mtu,wanafunzi wenzako,walimu,wafanyakazi wasio walimu,wanakijiji na viongozi wote.

Sheria na kanuni muhimu za shule

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kutumia busara(common sense)katika maisha yote awapo shule.
2. Wanafunzi lazima wawe na heshima na utu kwa watu wazima na wengine na kati yao wenyewe.
3. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza na kuangalia mali ya shule ya yake binafsi.
4. Wanafunzi hawaruhusiwi kufika nyumbani kwa walimu bila ruhusa ya matroni.

Scanned by CamScanner

5. Ni marufuku kuingia katika nyumba za starehe kama vile Baa,dansi na nyumba za kulala wageni(Guest house).
6. Ni wajibu wa mwanafunzi kutunza mazingira ya shule ,madarasa,vyoo na vyumba vingine shuleni katika hali ya usafi.
7. Matusi ya kusema au kuandika na ugomvi ni marufuku shuleni .
8. Mwanafunzi ni lazima ahudhurievipindi kwa masomo yote.Aidha ni lazima kuhudhuria vipindi vya dini yake kila siku kadri ya ratiba iliyopangwa.
9. Ni mwiko kwa mwanafunzi kujiunga na vikundi nyenye tabia mbaya popote pale na nje ya shule.
10. Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi shuleni kwa muda ulipangwa.
11. Ni marufuku kupokea wageni wa kwako binafsi uwapo shuleni.
12. Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya shule bila ruhusa.
13. Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele awapo darasani .
14. Mwanafunzi atunze nywele zake zikiwa fupi.Ni marufuku kuweka dawa (curl au relaxer) kwenye nywele.
15. Ni marufuku mwanafunzi kufuga kucha ndefu na kuwa na nywele ndefu.Mwanafunzi haruhusiwi kunyoa kipara,panki na kutinda nyusi za macho/usoni.
16. Mwanafunzi anapaswa avae sare wakati wote awapo shule na nje ya shule.
17. Urafiki wa mwanafunzi wa kike na kiume uwe ule wa kaka na dada.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi.
ii. Uasherati na ushoga.
iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine,mirungi kubeli na n.k.
iv. Kupigana au kumpiga mwanafunzi mwenzake,mwalimu au mlezi wake.
v. Kuharibu kwa makundi mali ya umma.
vi. Kudharau Bendera ya Taifa.
vii. Kuoa au kuolewa.
viii. Kupata mimba kutoa mimba ndani na nje ya shule.
ix. Kugoma,kuchochea migomo kuongoza na kuvuruga amani na

Scanned by CamScanner

usalama wa shule.

x. Dharau au kukataa adhabu kwa makusudi .
xi. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
xii. Utoro wa muda mrefu hadi muda wa siku tisini mfululizo.
xiii. Kosa lolote kubwa ambalo uongozi wa shule utaamua mwanafunzi anastahili adhabu kama hiyo .

VIAMBATANISHO

Pamoja na barua hii na ambatanisha

i. Fomu ya kupimwa na daktari
ii. Ahadi ya mzazi na mwanafunzi
iii. Historia na maelezo ya mwanafunzi

Mwisho

Ni imani yangu kuwa utasoma kwa makini/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu karibu sana Dutwa

Wako

.....

Mary Makalwe
MKUU WA SHULE
THE HEADMISTRESS
DUTWA SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 200 KARIADI

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA 0766 366 912

NAKALA:

1. MKURUGENZI ELIMU SEKONDARI
   S.L.P 9121
   DAR ES SALAAM
2. MKAGUZI WA SHULE KANDA
   KANDA YA MAGHARIBI
   S.L.P 1025
   TABORA
3. AFISA ELIMU (M)
   S.L.P 4
   SIMIYU
4. AFISA ELIMU SEKONDARI(W)
   S.L.P 109
   BARIADI

Scanned by CamScanner

SEHEMU B: FOMU YA MAMBO BINAFSI (PERSONAL PARTCULARS) IJAZWE KWA HERUFI KUBWA

1. Jina la mwanafunzi .....
2. Tarehe ya kuzaliwa .....mwezi.....mwaka.....
3. Uraia .....Kabila.....
4. Anuani kamili ya nyumbani(yaani wazazi/walezi

.....
.....
.....

Taja mahali ambapo mwanafunzi ataishi wakati wa masomo

5. Dini yake .....dhehebula .....

Jina la Baba/ .....Hai/sio.....
Jina la mama.....Hai/sio.....
Kazi ya Baba.....
Baba /mama/Mlezi anaishi
kijiji/mtaa.....wilaya.....Mkoa.....
Namba za simu ya
Baba/Mama/Mlezi.....
Kama anatunzwa na mlezi uhusiano ulionao na mlezi wako.....
Taja tatizo la kiafya/maumbile ulilo nalo(onesha na ambatanisha kivuli cha cheti kama
kipo.....

6. Andika majina ya ndugu ambao watashughulikia matatizo ya mwanafunzi

NA	JINA LA NDUGU	ANUANI	NAMBA YA SIMU	UHUSIANO NA MWANAFUNZI
1				
2				
3				
4				

Scanned by CamScanner

7. Maelezo ya nyongeza kama yapo :

.....

.....

.....

.....

SEHEMU C: FOMU YA KUPIMWA NA DAKTARI

(Nenda na fomu hii kwa daktari/Mganga katika Hospital ya Mkoa au Wilaya ili akupime na kukujazia ipasavyo)

Shule ya sekondari Dutwa
S.L.P 299,
BARIADI
TAREHE.....

Daktari/Mganga wa Mkoa wa mkoa/Wilaya

.....

.....

.....

MEDICAL CERTIFICATE

1. Jina la mwanfunzi .....
2. Kidato cha .....mwaka .....
3. Nimempima mtajwa hapo juu na amepatikana na ugonjwa wa .....na amepatiwa/hakupatiwa matibabu ipasavyo
4. Nimempima mtajwa hapo juu na kumuona hawezi kuendelea na masomo ya sekondari kwa sababu (kwa wasichana tu)imebainika kuwa ana/hana mimba ya miezi .....
5. **AFYA KWA UJUMLA**
   a) Kifua .....
   b) Macho.....
   c) Akili.....
   d) Kilema chochote (kitaje).....
   e) Mkojo.....
   f) Choo(stool).....
   g) Maradhi mengineyo(yataje).....
   .....
   .....

Jina la Daktari/Mganga .....sahihi .....tarehe.....

Scanned by CamScanner